Nishapona

Harmonize

Imani nafsi inaniambia
Haukuwa fungu langu
Na sidhani kama nilikosea
Kuukabidhi moyo wangu

Ulinidanganya mapenzi ni zuri basi
Panda twende safari
Bila kujua la kwako ni mwendo kasi
Ghafla ukanipa ajali

Upweke umetawala nafsi
Mwenzako usiku silali
Ninahesabu mabati
Kisa wewe

Sijutii moyo wangu
Kupenda nisipopendwa
Sirudii makosa yangu
Ujinga wakati wakwenda

Kinachoniuma roho yangu ooh
Kuwapa neno wahenga
Maana si kwa posti zangu
Na kujinadi napendwa

Nishapona, nishapona
Nishapona ila mazoea
Basi nenda umwambie

Nishapona!
Oooh mwambie
Basi umwambie eeh
Nishapona ila mazoea

Heshima kunyenyekea
Nilivyomnyenyekea
Akaniona si chochote kwake
Mazima akanipotezea
Akanipotezea, alipomaliza shida zake

Na bado siamini kweli ndo yule
Alokuwa akisema, halali asiponiona
Na kujilisha ya nini? Yote ni bure
Nikamwita chanda chema, alinidanganya

Zile miziki za kunichombeza, zinaniuma roho
Mara akinidekeza, elaji njoo
Ungesema nilipoteleza, nikamwomba koo
Si vyema amenitelekeza mb kisadooo

Basi nenda umwambie, nishapona!
Oooh mwambie
Basi umwambie eeh
Nishapona ila mazoea

Basi nenda umwambie, Nishapona!
Oooh mwambie

Basi umwambie eeh
Nishapona ila mazoea

Nenda kamwambie naja
Nenda kamwambie naja
Basi nenda kamwambie naja
Nenda kamwambie naja

Sponzor: www.srovnavac.cz - vyberte si pojištění online!